

HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

S.L.P 688
MPANDA
KATAVI

Barua pepe: info@nsimbodc.go.tz
Tovuti: www.nsimbodc.go.tz



Press No.NDC/ICTU/Press 45

May 27, 2019

TAARIFA KWA UMMA KUSITISHA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI NA KUANZA KUTUMIA MIFUKO MBADALA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inawatangazia Wananchi wote kuwa kuanzia Juni 1, 2019 Serikali itasitisha rasmi matumizi ya mifuko ya Plastiki na badala yake imeelekeza mbadala wa mifuko hiyo.

Mifuko mbadala inayotakiwa kutumika kama mbadala wa Mifuko ya Plastiki kuanzia Juni 1, 2019 ni pamoja na Mifuko iliyotengenezwa kwa Vitambaa, Karatasi, Gunia pamoja na Matumizi ya Vikapu ambayo ni rafiki kwa Mazingira.

Katika kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inatekeleza agizo hilo la Serikali Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imekwisha toa maelekezo katika ngazi ya Vijij kwa ajili ya kuandaa sehemu za kuhifadha mifuko itakayokusanywa katika maeneo hayo.

Maeneo yaliyoandaliwa kwa ajili ya kukusanyia Mifuko ya Plastiki ni pamoja na Ofisi za Watendaji wa Vijiji vyote 59 vya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Ofisi za Watendaji wa Kata, Shule za Sekondari, na Makao Makuu ya Halmashauri.

Hivyo Wananchi wote, pamoja na Wauzaji wote mnatakiwa kusitisha mara moja matumizi ya Mifuko ya Plastiki na usambazaji wa bidhaa hiyo haraka kabla ya Mwezi Juni 1, 2019 ili kuepuka usumbufu.

Aidha Wananchi wote mnatakiwa kukusanya mifuko hiyo ya Plastiki kwenye vituo vilivyoainishwa na Halmashauri ambapo hatua kali zitachukuliwa ikiwemo Faini na kifungo Gereza dhidi ya wale watakaokaidi utekelezaji wa zoezi hilo.

“OKOA MAZINGIRA, LINDA AFYA YAKO, TUMIA MIFUKO MBADALA”

Imetolewa na;

**KITENGO CHA TEKNOLOJIA YA HABARI MAWASILIANO NA UHUSIANO,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**